

Tindikali ni nini ?

Tindikali ni aina ya kemikali ambazo zina tabia ya kuunguza na kusababisha madhara kwa afya ya binadamu na mazingira. Mfano wa Tindikali ni kama vile Sulphuric acid ambayo pia hutumika kama maji makali ya betri.

Faida za Tindikali:

Tindikali ni muhimu katika maisha yetu ya kila siku, hutumika katika matumizi mbali mbali kama kutengeneza:

- Maji ya betri
- Rangi za nyumba na nguo
- Kemikali za kufanyia usafi
- Mbolea
- Wino
- Milipuko, na pia
- Uchunguzi kwenye Maabara

Madhara ya Tindikali:

Faida za tindikali ni nyingi lakini zisipodhibitiwa katika kila hatua na zisipotumiwa ipasavyo zinaweza kuleta madhara makubwa kwa afya ya binadamu na mazingira.

Mifano ya madhara ya tindikali kwa muda mfupi na muda mrefu kwa afya ya binadamu na mazingira ni:

- Kuunguza ngozi



- Mzio ("allergy") katika ngozi



- Kuharibu macho
- Kuharibu mfumo wa upumuaji kwa kuvuta hewa ya tindikali
- Kuharibu figo, moyo na mapafu
- Kuharibu mfumo wa uzazi
- Kusababisha kilema cha kudumu
- Kifo
- Kuathiri udongo hivyo vitu kama majengo, mabomba huathirika pia.
- Kuathiri maji hivyo kupelekea viumbe hai wa majini kufa kama vile samaki.
- Kuondoa virutubisho kwenye udongo vinavyosaidia ukuaji wa mimea hivyo kudumaza ukuaji wa mimea.


Huduma ya kwanza kabla ya kumuona daktari baada ya kupata tatizo dhidi ya tindikali:

- Imeingia machoni: osha kwa maji mengi kwa muda wa dakika 15.
- Imemwagika kwenye ngozi: Osha kwa maji mengi na sabuni ya kuua vijidudu eneo lililo athirika.
- **Imenywewa:** Usimtapishe mtu aliyekunywa tindikali na asipewe kitu chochote kula.

- Amevuta hewa ya tindikali: Apelekwe kwenye hewa safi, kama anapumua kwa shida tumia kifaa cha kupumulia(oxygen), au kumsaidia kutoa pumzi kwa kutumia mdomo ("mouth to mouth resuscitation")

Jinsi ya kuitunza Tindikali:

- Chombo cha kutunza tindikali kiwe kikavu na kuhifadhiwa mahali salama pasipo na unyevunyevu.
- Chombo cha kutunza tindikali kifungwe vizuri bila kupitisha hewa na fungua kwa uangalifu bila kutingisha.
- Unapoifungua tindikali hakikisha umevaa vifaa vya kujikinga kama maski ya kuchuja hewa ya sumu, glovu na miwani.



Angalizo:

- Wadau wote wanaojishughulisha na matumizi ya tindikali wahakikishe wamejisajili kwa Mkemia Mkuu wa Serikali kufuatana na Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Kemikali za Viwandani na Majumbani Na. 3 ya mwaka 2003 Sura 182.
- Wenye magari wajaze maji ya betri kwa waliosajiliwa na Mkemia Mkuu wa Serikali.
- Tindikali isitunzwe majumbani.
- Tindikali isisafirishwe kwenye magari ya abiria.

Kwa maelezo zaidi wasiliana na:

Mkemia Mkuu wa Serikali
Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali
Luthuli/ Barack Obama Drive
S.L.P. 164

Dar Es Salaam, Tanzania

Simu: + 255 22 2113383/4

Nukushi: +255 22 2113320

Baruapepe: cgc@gcla.go.tz, gcla@gcla.go.tz

Meneja

Maabara ya Kanda ya Mashariki

Luthuli/Barack Obama Drive

S.L.P. 164

Dar Es Salaam, Tanzania

Simu: + 255 22 2113383/4

Nukushi: +255 22 2113320

Baruapepe: gcla.east@gcla.go.tz

Meneja

Maabara ya Kanda ya Ziwa,

Eneo la Hospitali ya Sekou Toure/Isamilo

S.L.P. 502,

Mwanza, Tanzania.

Simu: +255 28 2500279

Baruapepe: gcla.lake@gcla.go.tz

Meneja

Maabara ya Kanda ya Kaskazini

Kituo cha Afya Themis

S.L.P. 2095

Arusha, Tanzania.

Simu: +255 27 2506394

Nukushi: +255 27 2549026

Baruapepe: gcla.north@gcla.go.tz

Meneja

Maabara ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini

Eneo la Hospitali ya Mkoa wa Mbeya

New Forest Area

S.L.P. 2875

Mbeya, Tanzania.

Simu: +255 25 2502311

Nukushi: +25525 250 312

Barua pepe: gcla.southern@gcla.go.tz

Meneja

Maabara ya Kanda ya Kusini

Ushirika House

Barabara ya TANU

S.L.P. 1414

Mtwara, Tanzania.

Simu: +255 23 233 4760

Nukushi: +255 23 233 4761

Barua pepe: gcla.south@gcla.go.tz

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII,
JINSIA, WAZEE NA WATOTO



WAKALA WA MAABARA YA
MKEMIA MKUU WA SERIKALI

ISO 9001:2008

ISO 17025:2005

IDARA YA SAYANSI JINAI NA
HUDUMA ZA VINASABA

TINDIKALI
(ACIDS)



SHERIA YA USIMAMIZI NA UDHIBITI WA
KEMIKALI ZA VIWANDANI NA MAJUMBANI,
Na. 3 YA MWAKA 2003 (SURA 182)